



**TALKING NOTES ZA MHE. THOBIAS E. M. ANDENGENYE, MKUU WA MKOA  
WA KIGOMA WAKATI WA KUFUNGUA MKUTANO WA UJIRANI MWEMA WA  
MAKAMANDA WA POLISI WA MIKOA YA TANZANIA INAYOPAKANA NA  
DR CONGO NA BURUNDI - TAREHE 30 NOVEMBA, 2021**

**UTANGULIZI**

SACP Geminis Mushy - Mwakilishi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania

ACP Joseph Manyama - Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma

Mhe. Theo Mwambu Mullasa - Balozi mdogo wa DR Congo

Mhe. Adalbert Nininahazwe - Balozi Mdogo wa Jamhuri ya Burundi

Kamishna wa Polisi - Mkoa wa Kivu Kusini,

Kamishna wa Polisi - Mkoa wa Tanganyika,

Kamishna wa Polisi - Mkoa wa Makamba

Kamanda wa Polisi - Mkoa wa Rukwa

Kamanda wa Polisi - Mkoa wa Katavi

Makamanda na Maafisa Mliopo,

Ndg. Wageni Waalikwa,

Ndg. Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

***Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!***



## Ndg.Mabibi na Mbwana,

- Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hapa Mkoani Kigoma kwa ajili ya kikao cha Ujirani Mwema cha Makamanda wa Polisi wa Mikoa jirani ya Nchi za Tanzania Burundi na DR Congo.
- Pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa mwaliko wa kushiriki na kuzungumza nanyi katika kikao hiki muhimu kinacholenga kujadili mustakabli wa masuala mbalimbali ya ulinzi na usalama katika nchi zetu.
- Aidha, naipongeza sana Serikali ya awamu ya Sita chini ya Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuweka na kuboresha miundombinu bora ya usafiri na mawasailiano ambayo kimsingi inawanufaisha Watanzania pamoja na Majirani zetu.
- Kikao hiki cha Ujirani Mwema cha Makamanda wa Polisi wa Mikoa jirani ya Nchi za Tanzania Burundi na DR Congo ni hatua njema kwa vyombo vyetu vya usalama kuahikisha utangamano wa Afrika mashariki unakua na kuleta fursa zamaendeleo kwa wananchi wetu kufanya kazi na biashara kwa uhuru zaidi ili kujiletea maendeleo. Kikao hiki ni moja ya



mikakati ya kukuza na kuendeleza utangamano wa afrika mashariki na ustawi wa watu wake ambao kimsingi ni ndugu.

- Suala la Ulinzi na Usalama katika ukanda wetu si suala la kuachia nchi moja au mkoa mmoja, ni jambo linalohitaji mashirikiano ya karibu kwa vyombo vyetu vya usalama ili kudhibiti uhalifu wa aina yoyote katika mipaka na ndani ya nchi zetu. Uhalifu hauna mipaka na hata mapambano ya kweli dhi ya uhalifu hayapaswi kuzuiwa na uwepo wa mipaka
- Kama mnavyofahamu katika maeneo mengi yanayotuzunguka matukio ya uhalifu ikiwemo ugaidi yameanza kujitokeza kwa njia mbalimbali. Kikao kama hiki ni muhimu kufanyika ili hata kama bado hayajaanza kutokea katika maeneo yetu basi tuwe na mikakati madhubuti ya kukabiliana na matukio kama hayo.
- Kama niivyosema hapo awali kuwa Uhalifu hauna mipaka na hata mapambano ya kweli dhi ya uhalifu hayapaswi kuzuiwa na uwepo wa mipaka. Makosa kama usafirishaji wa dawa za kulevyta, usafirishaji wa mali ya wizi, biashara ya silaha, na bidhaa bandia, huduma haramu (ngono ya kibashara na usafirishaji haramu wa binadamu), na upenyezaji wa biashara na serikali (udanganyifu, utapeli, utakatishaji fedha, na ufisadi) yameendelea kuathiri nchi nyingi. Ni masuala yanayohitaji ushirikiano wa pamoja katika kukabiliano nayo.



- Aidha, matukio ya kihalifu ikiwemo ujambazi na wizi wa kutumia silaha nao umeshuhudiwa mara kadhaa katika maeneo yetu ya mipakani, sambamba na usafirishwaji wa silaha kinyemela. Haya yote yanafanywa na wananchi kutoka katika nchi zetu, mikoa na maeneo yetu. Hivyo ninaamini kikao hiki kitatoka na maazimio mathubuti ambayo yatasaidia kuweka utaratibu mzuri wa kushirikiana katika kukabiliana na wahalifu/uhalifu unaovuka mipaka kwa nia ya kukomesha ama kupunguza kasi ya matukio kama hayo.
- Uhamiaji haramu nao umeshika kasi ambapo watu wengi wanahama maeneo yao na kuingia mipaka ya nchi nyingine kwa kutumia njia zisizo sahihi kisheria. Hata hivyo baadhi ya wahamiaji haramu wamekuwa wakikamatwa zaidi ya Mara moja kwa kufanya makosa hayo. Katika kikao hiki tuone na kuweka mipango mikakati ya kupunguza uhamaji haramu na kuwataka wananchi kufuata sheria na taratibu za mtu kuvuka mipaka.
- Natoa msisitizo kwamba vikao kama hivi tuone namna ya kuvifanya viwe endelevu ili kuwepo na uhai wa namna ya kushirikiana katika kuimarisha suala la ulinzi na usalama katika ukanda wetu. Tunapoimarisha usalama katika ukanda huu ndipo tunatoa fursa kwa wananchi wetu kukuza uchumi kwa kufanya shughuli za uzalishaji bila bugudha.



- Kabla ya kufikia tamati, naomba niwakaribishe sana wale wageni katika Mkoa wa Kigoma. Baada ya kikao hiki mnawenza kutembelea mji wa Kigoma na maeneo mbalimbali ya kutalii kama Mahale, na Gombe ili mjonee madhari nzuri ya Mkoa wa Kigoma.
  
- Baada ya kusema hayo natamka kuwa kikao cha Ujirani mwema cha Makamada wa Polisi wa Mikoa ya Rukwa, Katavi, Kigoma, Kivu kusini, Tanganyika na Makamba sasa nimekifungua rasmi.

**Akhsanteni kwa Kunisikiliza.**